

# CHUO KIKUU CHA MTAKATIFU AGUSTINO TANZANIA

## S.L.P 307 MWANZA, TANZANIA



### TAARIFA KWA UMMA

---

Kutokana na taarifa iliyotolewa na vyombo mbalimbali vya habari tarehe 20/06/2022 kuhusu mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania (SAUT) bewa kuu la Mwanza kunusurika kipigo kutoka kwa wananchi wenye hasira baada ya kujifungua mtoto na kisha kumtupa nyuma ya nyumba anayoishi, Uongozi wa Chuo kupitia Ofisi ya Mlezi wa Wanafunzi ilifuatilia suala hilo ambalo kwa sasa lipo kwenye mamlaka za Jeshi la Polisi kwa uchunguzi zaidi.

Kwa taarifa za awali, mwanafunzi aliyehusishwa na tukio hilo (jina lake limehifadhiwa kwa sababu za kiusalama) anasoma fani ya Sheria mwaka wa tatu chuoni hapa. Taarifa ya Jeshi la Polisi inaeleza kuwa mwanafunzi huyo anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando baada ya kukutwa katika hali mbaya kiafya kutokana na changamoto za kujifungua.

Aidha, Chuo kinasubiri taarifa ya kitabibu kutoka hospitalini na kisha kutoa mwongozo wa taratibu zitakazofuata baada ya jeshi la Polisi na mamlaka nyingine za kisheria kukamilisha uchunguzi wake.

Tunatoa rai kwa jamii ya wanafunzi kutilia maanani dhumuni la msingi la kuwapo chuoni hususan kuzingatia masomo, maadili na kutojiingiza katika makundi hatarishi. Tukio la namna hiyo linaweza kukatisha ndoto za wanafunzi na kutokuwa na tija na msaada kwa familia zao, jamii na taifa kwa ujumla.

**Imetolewa na**  
**Ofisi ya Uhusiano - SAUT**  
**23/06/2022**